PRESS RELEASE

ISSUED BY INFORMATION SERVICES DIVISION

MINISTRY OF INFORMATION AND TOURISM

P. O. BOX 9142 DAR ES SALAAM TELEPHONE 20656

TIS

UNIV. COLLEGE DAR ES SALAAM LIBRARY

A/162/67
IT/I.326

Januari 29, 1967
(Saa $10\frac{1}{4}$ alasiri)

RAIS NYERERE AWEKA JIWE LA MSINGI LA
CHUO CHA POLISI - MOSHI

Rais wa Tanzania, Mwalimu Julius K.Nyerere leo alipokelewa kwa shangwe na maelfu ya wananchi wa mjini Moshi wakati alipowasili kwa motokaa toka Arusha.

Mara baada ya kuwasili, Mwalimu aliweka jiwe la msingi la Chuo cha kufundishia askari polisi mjini Moshi. Gharama ya Chuo hicho pamoja na nyumba 91 zikiwa ni pamoja na nyumba za watumishi na mabweni ya wanafunzi, itakuwa shilingi 8 milioni. Nusu ya fedha hiyo ni msaada toka serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. Kazi ya kujenga Chuo hicho imeanza; na hivi sasa mafundi wa Kichina wanasaidia ujenzi wa Chuo hicho. Inafikiriwa kwamba kazi hiyo itamalizika kati ya mwezi Julai na Agosti mwaka ujao (1968).

Hapo mapema Mwalimu Mkuu wa shule ya kufundishia askari polisi mjini Moshi, Bwana G.Sawaya alisoma taarifa fupi juu ya maendeleo ya shule hiyo tangu ilipohamishwa toka Morogoro katika mwaka 1923.

Baadaye Balozi wa China katika Tanzania, Bwana Ho Ying, katika hotuba fupi aliyotoa kwenye sherehe hiyo, alisifu juhudi za wananchi wa Tanzania katika kulijenga Taifa lao chini ya uongozi wa Rais Nyerere; na akasifu pia siasa ya Kujitegemea wenyewe. Alisema kuwa wananchi wa China, chini ya uongozi wa Mwenyekiti Mao Tse Tung, wanaunga mkono Watanzania katika jitihada zao za kuijenga nchi yao; na kwamba kila mara wako tayari kuwasaidia katika shughuli za kuliendeleza Taifa.

Baadaye Rais akifuatana na Waziri wa Nchi, Bwana Bhoke Munanka, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Bwana L.N.Sijaona, Waziri wa Ardhi, Makazi na Maji, Bwana S.A.Maswanya, alikagua baadhi ya majengo ya Chuo hicho, kabla ya kuondoka kwa motokaa kwenda Same ambako alikula chakula cha mchana.

Mwalimu alikabidhiwa shilingi 305/- na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Bwana A.W.Mwakang'ata zikiwa ni mchango kwa Watoto Yatima toka kwa watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilimanjaro.

Rais Nyerere ameondoka Same leo mchana kwa motokaa kwenda Tanga.

- mwisho-